

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**



**MTAALA WA ELIMU YA SEKONDARI**  
**KIDATO CHA V-VI**

**2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023

Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-838-5

Taasisi ya Elimu Tanzania  
Eneo la Mikocheni  
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi  
S.L.P 35094  
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170  
Baruapepe: [director.general@tie.go.tz](mailto:director.general@tie.go.tz)  
Tovuti: [www.tie.go.tz](http://www.tie.go.tz)

Mtaala huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Mtaala wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishina wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## Yaliyomo

|  |      |
|--|------|
| Orodha ya Majedwali.....                                     | v    |
| Vifupisho.....   | vi   |
| Shukurani.....   | vii  |
| Dibaji.....  | viii |
| Sehemu ya Kwanza.....  | 1    |
| Utangulizi.....  | 1    |
| 1.1 Usuli.....   | 1    |
| 1.2 Muundo wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI.....        | 1    |
| Sehemu ya Pili.....  | 2    |
| Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla.....                       | 2    |
| 2.1 Dira ya Elimu ya Tanzania.....                           | 2    |
| 2.2 Malengo Makuu ya Elimu ya Tanzania.....                  | 2    |
| 2.3 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI.....       | 2    |
| 2.4 Umahiri wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI.....       | 3    |
| Sehemu ya Tatu.....  | 4    |
| Maudhui ya Mtaala.....                                       | 4    |
| 3.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo.....                      | 4    |
| 3.2 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo.....            | 5    |
| 3.3 Maeneo ya Ujifunzaji na Tahasusi za Kidato cha V-VI..... | 30   |
| Sehemu ya Nne.....   | 38   |
| Ufundishaji na Ujifunzaji.....                               | 38   |
| 4.1 Muda na idadi ya vipindi.....                            | 38   |
| 4.2 Lugha ya Kufundishia na Kujiifunzia.....                 | 38   |
| Sehemu ya Tano.....  | 39   |
| Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji na Ujifunzaji.....        | 39   |
| 5.1 Upimaji endelevu.....                                    | 39   |
| 5.2 Upimaji tamati.....                                      | 39   |

|   |    |
|---|----|
| 5.3 Zana na mbinu za upimaji na tathmini .....                        | 40 |
| Sehemu ya Sita.....   | 41 |
| Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala.....                              | 41 |
| 6.1 Rasilimali watu.....  | 41 |
| 6.2 Rasilimali vitu .....   | 41 |
| 6.3 Samani na majengo .....   | 41 |
| 6.4 Rasilimali muda.....  | 42 |
| 6.5 Rasilimali fedha.....   | 42 |
| 6.6 Ushiriki wa Wadau katika Utekelezaji wa Mtaala .....              | 42 |
| 6.7 Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mtaala ..... | 42 |
| Bibliografia .....  | 43 |

## Orodha ya Majedwali

|   |    |
|---|----|
| <b>Jedwali 1:</b> Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI .... | 4  |
| <b>Jedwali 2:</b> Mchanganuo wa Masomo, Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi.....               | 5  |
| <b>Jedwali 3:</b> Maeneo ya Ujifunzaji na Tahasusi za Kidato cha V-VI.....                  | 34 |
| <b>Jedwali 4:</b> Mgawanyo wa Muda na Vipindi.....  | 38 |
| <b>Jedwali 5:</b> Mchanganuo wa alama za upimaji endelevu.....                              | 39 |

## Vifupisho

|        |  |
|--------|--|
| LAT    | Lugha ya Alama ya Tanzania                                       |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano                              |
| TET    | Taasisi ya Elimu Tanzania  |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation |
| WyEST  | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia                           |

## Shukurani

Maandalizi ya Mtaala wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI yamehusisha wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha upatikanaji wa mtaala huu. Hivyo, TET inatoa shukurani za dhata kwanza, kwa Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb.). Kamati hiyo ilikuwa na wajumbe 10, wakiongozwa na Mwenyekiti wake Prof. Makenya Abraham Maboko. Kamati hii ilifanya kazi kwa bidii kubwa na hatimaye kuhakikisha kuwa mtaala huu unaandaliwa kwa wakati na unakidhi shauku ya wadau juu ya ubora wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI .

Pili, shukurani ziende kwa taasisi, wizara na wadau mbalimbali wa elimu walioshiriki kutoa maoni kuhusu uboreshaji wa mtaala. Baadhi ya taasisi, wizara na wadau hao ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wajumbe wa Kamati ya Mapitio ya Sera ya Elimu, wajumbe wa Kamati ya Kufanya Mageuzi Makubwa ya Elimu Zanzibar, Viongozi wa dini, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Taasisi ya Elimu Zanzibar, Bodi na Manajimenti za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania, menejimenti na wakufunzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Chuo cha Amali Zanzibar, Baraza la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi, Baraza la Mitihani Tanzania, Chama cha Walimu Tanzania, Baraza la Watoto na Vijana Balehe Tanzania. Vilevile, wadau wengine ni wajumbe wa bodi za shule, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, walimu wa shule za msingi, sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wahadhiri wa vyuo vikuu, waajiri, wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu, Tume ya Vyama vya Ushirika, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Akademia ya Sayansi Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania na Shirika la Chakula na Kilimo la Kimataifa.

Tatu, TET inayashukuru mashirika ya *United Nations International Children's Fund, United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation, Room to Read, Right to Play, Data Vision, Plan International, Norwegian Refugees Council, Christian Social Services Commission, Global Education Link, UWEZO, Hill Packaging Ltd., Teacher Education Support Project, Madrasa Early Childhood Programme – Zanzibar, Morale Foundation for Education and Training na Educate* kwa kufadhili hatua mbalimbali za uandaaji wa mitaala.

Nne, TET inatoa shukurani za dhata kwa wataalamu wote wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI kutoka ndani na nje ya TET walioshiriki kuandaa mtaala huu. Mwisho, ingawa si kwa umuhimu, TET inaishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kuwezesha kazi ya uandishi, uchapaji na usambazaji wa mtaala huu.



Dkt Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## Dibaji

Mtaala wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI umeandaliwa kwa kuzingatia *Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014* Toleo la Mwaka 2023, maoni ya wadau yaliyokusanywa na kuchakatwa kuanzia mwaka 2021 hadi 2022 na matokeo ya uchambuzi wa maandiko kuhusu uzoefu kutoka nchi nyingine. Aidha, mtaala huu unazingatia Dira ya Elimu ambayo inalenga kumwandaa Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, mtaala huu umezingatia malengo makuu ya elimu pamoja na malengo ya elimu ya msingi nchini Tanzania. Kwa kuzingatia haya, mtaala huu umeweka viwango vya utoaji wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI kwa kubainisha ujuzi, maarifa, stadi na mwelekeo atakaoujenga mwanafunzi, umahiri wa jumla, maeneo makuu ya ujifunzaji, umahiri mkuu na mahususi, njia za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, mtaala umebainisha muda utakaotumika katika utekelezaji, lugha ya kujifunzia na kufundishia, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na njia zitakazotumika katika upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Vilevile, mtaala umebainisha sifa za kitaaluma na kitaalamu za mwalimu ambaye ndiye mtekelezaji mkuu wa mtaala katika ngazi ya shule.

Pamoja na matamko mbalimbali ya kisera na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa, mtaala huu umezingatia nadharia za ujifunzaji na Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea. Falsafa hiyo inasisitiza utoaji wa elimu inayomwezesha Mtanzania kujitegemea na kumudu maisha yake ya kila siku. Ni matarajio yangu kuwa kupitia mtaala huu, mwalimu atamwezesha mwanafunzi kujenga umahiri uliokusudiwa. Pia, wasimamizi wote wa utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI na wadau wengine nchini watahakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa.



Dkt Lyabwene M. Mtahabwa  
**Kamishna wa Elimu**



# Sehemu ya Kwanza

## Utangulizi

### 1.1 Usuli

Nchi nyingi duniani, ikiwemo Tanzania, zinatambua kwamba elimu ni haki ya kila mtu na hivyo zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa kwa haki na usawa. Jitihada hizi zinafanyika kutokana na ukweli kwamba elimu ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya kila binadamu kitaaluma, kimaadili na katika ukuzaji wa vipaji na vipawa mbalimbali. Kutokana na azma ya Taifa ya kujenga nchi yenye uchumi shindani kitaifa na kimataifa, Serikali imelenga kujenga jamii yenye maarifa, stadi na mwelekeo chanya itakayoweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kimaendeleo.

Tanzania imejizatiti kutoa elimu bora na jumuishi inayozingatia Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea iliyoasisiwa mwaka 1967 na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Aidha, mtaala huu wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI umejikita katika ujenzi wa umahiri wa msingi katika Stadi za Karne ya 21 ambazo ni kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali, maadili na uzalendo. Hivyo basi, mtaala huu umeandaliwa kwa lengo la kuwandaa Watanzania wenye maarifa, stadi na mtazamo chanya katika kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya Karne ya 21.

Uandaaji wa Mtaala huu umepitia hatua mbalimbali ikiwemo; kukusanya maoni ya wadau, mapitio ya nyaraka mbalimbali na kujifunza uzoefu kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kujifunza mifano bora inayoweza kutekelezeka katika mazingira ya Tanzania.

### 1.2 Muundo wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI

Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI itatolewa kwa muda wa miaka miwili (2), kama inavyoelekezwa na *Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014* Toleo la Mwaka 2023. Mwanafunzi atanza Kidato cha V akiwa na umri wa miaka 16 na kuhitimu Kidato cha VI akiwa na umri wa miaka 17. Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI imejikita kwenye masomo ya jumla yatakayotolewa katika tahasusi ili kumwandaa mhitimu kujiunga na elimu ya juu. Mwanafunzi atachagua tahasusi kulingana na matakwa yake, uwezo na malengo yake ya maisha. Aidha, pamoja na masomo ya tahasusi, mwanafunzi atachukua masomo mawili ya lazima ambayo ni Mawasiliano ya Kitaaluma na Historia ya Tanzania na Maadili. Mwanafunzi ambaye hasomi somo la Hisabati na ambaye anasoma masomo ya sayansi, uchumi na uhasibu atalazimika pia kusoma somo la *Basic Applied Mathematics*. Iwapo Mwanafunzi atasoma somo la *Additional Mathematics* katika ngazi ya sekondari ya chini na kufaulu hatalazimika kusoma somo la *Basic Applied Mathematics*.

## **Sehemu ya Pili**

### **Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla**

Mtaala huu umezingatia dira, malengo na umahiri unaotakiwa kujengwa kwenye hatua ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI kama ilivyofafanuliwa katika Dira ya Elimu ya Tanzania, Malengo Makuu ya Elimu ya Tanzania, Malengo Mahususi na Umahiri wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI.

#### **2.1 Dira ya Elimu ya Tanzania**

Dira ya Elimu ya Tanzania ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa.

#### **2.2 Malengo Makuu ya Elimu ya Tanzania**

Malengo makuu ya elimu ya Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

- (a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
- (b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
- (c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
- (d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;
- (e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
- (f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
- (g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
- (h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

#### **2.3 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI**

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI ni kumwezesha mwanafunzi:

- (a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi, na mwelekeo alioupata katika ngazi ya elimu ya Sekondari Hatua ya Chini;

- (b) Kulinda mila na desturi, tunu za Taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, na wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;
- (c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi;
- (d) Kuimarisha matumizi ya lugha katika mawasiliano ya kitaaluma;
- (e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia, na utunzaji endelevu wa mazingira;
- (f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na
- (g) Kumwandaa mwanafunzi kujiunga na vyuo vya elimu ya kati.

#### **2.4 Umahiri wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI**

Umahiri wa Jumla unatarajiwa kumjenga mwanafunzi kumudu mambo yafuatayo:

- (a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika ngazi ya elimu ya Sekondari Hatua ya Chini kuimarisha na kupanua uelewa wake wa elimu ya jumla;
- (b) Kuthamini uraia, tunu za Taifa, na haki za binaadamu na za kiraia;
- (c) Kujiamini katika ujifunzaji wa nyanja mbalimbali zikiwemo Sayansi na Teknolojia, maarifa ya kinadharia na ya kivitendo;
- (d) Kutumia stadi za lugha katika kufanya mawasiliano ya kitaaluma;
- (e) Kutumiamaarifayamasualamtambukakumudumazingirayanayomzunguka;
- (f) Kutumia ujuzi na stadi alizozipata kumwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na
- (g) Kuonesha utayari wa kujiunga na elimu ya ngazi inayofuata.

## Sehemu ya Tatu

### Maudhui ya Mtaala

Maudhui ya Mtaala wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI yanajumuisha maeneo ya ujifunzaji, masomo, umahiri mkuu na umahiri mahususi. Maudhui haya yamefafanuliwa kama ifuatavyo:

#### 3.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo

Maeneo ya ujifunzaji na masomo yatakayofundishwa Kidato cha V-VI yamezingatia umahiri wa jumla uliofafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya mtaala huu na yameainishwa katika Jedwali 1.

**Jedwali 1:** Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ya Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI

| S/N | Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo   |
|-----|----------------------|--|
| 1   | Sayansi Jamii        | 1. Historia<br>2. Jiografia<br>3. Elimu ya Dini ya Kikristo<br>4. Elimu ya Dini ya Kiislamu<br>5. Historia ya Tanzania na Maadili*   |
| 2   | Lugha na Fasihi      | 6. Kiswahili<br>7. English<br>8. Lugha ya Kiarabu<br>9. Lugha ya Kifaransa<br>10. Lugha ya Kichina<br>11. Mawasiliano Kitaaluma*<br>12. Fasihi ya Kiswahili<br>13. Literature in English |
| 3   | Sayansi Asilia       | 14. Fizikia<br>15. Kemia<br>16. Baiolojia<br>17. Kilimo<br>18. Chakula na Lishe  |
| 4   | Hisabati             | 19. Hisabati<br>20. Hisabati Tumizi*   |
| 5   | Teknolojia           | 21. Sayansi ya Kompyuta  |
| 6   | Biashara na Uchumi   | 22. Uchumi<br>23. Biashara<br>24. Uhasibu  |

|   |                             |   |
|---|-----------------------------|---|
| 7 | Utamaduni, sanaa na michezo | 25. Sanaa Sanifu<br>26. Muziki<br>27. Sanaa za Maonyesho<br>28. Ushoni<br>29. Michezo |
|---|-----------------------------|---|

\*Masomo yasiyo ya tahasusi

### 3.2 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo

Umahiri mkuu na umahiri mahususi atakaojengewa mwanafunzi umeainishwa kwa kila somo. Mwanafunzi wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI atajengewa umahiri ulioainishwa katika Jedwali 2.

**Jedwali 2:** Mchanganuo wa Masomo, Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

| Na | Somo     | Umahiri Mkuu  | Umahiri Mahususi   |
|----|----------|---|--|
| 1. | Historia | 1.1 Kumudu historia ya umajumui wa Afrika           | 1.1.1 Kumudu dhana ya umajumui wa Afrika na chimbuko lake katika Karne ya 15<br>1.1.2 Kuelezea umajumui wa Afrika katika Karne ya 16 hadi 19<br>1.1.3 Kuthamini historia ya umajumui wa Kiafrika wakati wa ukoloni na mapambano dhidi ya ukoloni, 1900-1960<br>1.1.4 Kuthamini umajumui wa Afrika kuanzia 1960 hadi sasa |
|    |          | 1.2 Kumudu historia ya mapinduzi ya viwanda duniani | 1.2.1 Kuchambua mapinduzi ya viwanda katika mataifa ya awali ya viwanda duniani, Karne ya 18 na 19<br>1.2.2 Kuchambua kukua kwa mapinduzi ya viwanda kuanzia Karne ya 20 hadi sasa<br>1.2.3 Kutathmini ukuaji wa viwanda Afrika  |

| Na | Somo | Umahiri Mkuu   | Umahiri Mahususi   |
|----|------|--|--|
|    |      | <p>1.3 Kutathmini historia ya mifumo mbalimbali ya utawala duniani</p> | <p>1.3.1 Kuelezea chimbuko la mifumo ya utawala kutoka enzi za kale</p> <p>1.3.2 Kuelezea mchango wa dini katika ujenzi wa mifumo ya sasa ya utawala</p> <p>1.3.3 Kutathmini namna mifumo ya utumwa na ukabaila ilivyoleta mabadiliko katika utawala</p> <p>1.3.4 Kuchambua namna mapinduzi ya kisiasa Ulaya yalivyochochea ukuaji wa mifumo mipya ya utawala</p> <p>1.3.5 Kutathmini namna migogoro ya kibepari ilivyozalisha itikadi na mifumo ya utawala mbadala katika Karne ya 20</p> <p>1.3.6 Kuchambua mifumo ya kiutawala iliyojengwa barani Afrika baada ya uhuru</p> |
|    |      | <p>1.4 Kutathmini historia ya matishio ya amani duniani</p>            | <p>1.4.1 Kuchambua mifano ya vita kubwa zilizopiganwa kuanzia Karne ya 17 hadi 19</p> <p>1.4.2 Kuchambua historia ya migogoro na vita katika Karne ya 20</p> <p>1.4.3 Kutathmini viashiria na matishio mapya ya amani duniani</p> <p>1.4.4 Kuchambua matishio ya amani duniani yatokanayo na vita vya kikabila</p>   |
|    |      | <p>1.5 Kumudu historia ya maendeleo barani Afrika</p>                  | <p>1.5.1 Kuelezea historia ya maendeleo ya Afrika baada ya ukoloni</p>   |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b>               | <b>Umahiri Mkuu</b>  | <b>Umahiri Mahususi</b>  |
|-----------|---------------------------|--|--|
|           |                           | 1.6 Kufanya kazimradi ya kihistoria  | 1.6.1 Kufanya kazimradi ya kihistoria  |
| 2.        | Jiografia                 | 2.1 Kumudu stadi za muundo wa dunia  | 2.1.1 Kukuza uelewa wa dhana na nadharia za muundo wa dunia<br>2.1.2 Kuonesha uelewa wa visababishi vya maumbile makuu ya sura ya dunia<br>2.1.3 Kuonesha uelewa wa miamba na mmeng'enyuko wake<br>2.1.4 Kumudu misingi ya haidrolojia |
|           |                           | 2.2 Kumudu stadi za kijiografia  | 2.2.1 Kumudu stadi za juu za usorovea<br>2.2.2 Kutafsiri ramani na picha<br>2.2.3 Kumudu stadi za utafiti wa kijiografia   |
|           |                           | 2.3 Kufanya kazimradi ya kijiografia                                       | 2.3.1 Kufanya kazimradi ya kijiografia   |
| 3.        | Elimu ya Dini ya Kikristo | 3.1 Kutumia Agano la Kale kumudu dhana za utawala bora, ujasiri na maamuzi | 3.1.1 Kukuza uelewa wa dhana ya utawala bora kwa kutumia vitabu vya Waamuzi, Samweli na Wafalme<br>3.1.2 Kukuza uelewa wa dhana ya ujasiri na maamuzi kutokana na maisha na kazi za manabii Eliya na Elisha                            |

| Na | Somo                      | Umahiri Mkuu  | Umahiri Mahususi  |
|----|---------------------------|---|---|
|    |                           | 3.2 Kumudu maandiko ya baadhi ya manabii na kuyahusianisha na maisha ya kila siku | 3.2.1 Kuonesha uelewa wa mafundisho ya Nabii Isaya<br>3.2.2 Kuonesha uelewa wa dhana za haki, upendo na huruma kwa kutumia maandiko ya manabii Amosi na Hosea<br>3.2.3 Kuonesha uelewa wa umuhimu wa uwajibikaji kwa kutumia maandiko ya manabii Hagai na Zakaria         |
|    |                           | 3.3 Kumudu baadhi ya maandiko katika Agano Jipya                                  | 3.3.1 Kumudu maandiko matakatifu katika Injili ya Mathayo<br>3.3.2 Kumudu maandiko matakatifu katika Injili ya Yohana<br>3.3.3 Kumudu maandiko matakatifu ya Waraka wa Mtume Paulo kwa Warumi<br>3.3.4 Kumudu maandiko matakatifu ya Waraka wa Mtume Yakobo kwa watu wote |
|    |                           | 3.4 Kufanya kazimradi katika Elimu ya Dini ya Kikristo                            | 3.4.1 Kufanya kazimradi katika Elimu ya Dini ya Kikristo  |
| 4. | Elimu ya Dini ya Kiislamu | 4.1 Kuishi kwa mujibu wa itikadi ya Uislamu                                       | 4.1.1 Kuchambua dhana ya Elimu kwa mtazamo wa Uislamu<br>4.1.2 Kuthibitisha usahihi wa Itikadi ya Uislamu<br>4.1.3 Kuthamini nguzo za Imani ya Kiislamu   |



| Na | Somo | Umahiri Mkuu   | Umahiri Mahususi   |
|----|------|--|--|
|    |      | 4.2 Kuthamini Qur'an na Sunnah   | 4.2.1 Kuthibitisha kuwa Qur'an ni maneno ya Allah (S.W)<br>4.2.2 Kuchambua misingi ya kufasiri Qur'an<br>4.2.3 Kuchambua dhana ya Sunnah<br>4.2.4 Kuchambua mambo mtambuka katika jamii kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah |
|    |      | 4.3 Kumtumikia Allah (S.W) katika nyanja zote za maisha                | 4.3.1 Kutathmini utekelezaji wa nguzo za Uislamu<br>4.3.2 Kutathmini mifumo ya maisha kwa mujibu wa Uislamu<br>4.3.3 Kufafanua misingi ya Sharia<br>4.3.4 Kuthamini matumizi ya Sharia katika miamala mbalimbali       |
|    |      | 4.4 Kuthamini historia katika kuimarisha Haki na Uadilifu katika jamii | 4.4.1 Kufafanua dhana ya Historia kwa mujibu wa Uislamu<br>4.4.2 Kutathmini historia ya Uislamu kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) hadi hivi sasa<br>4.4.3 Kujenga mwenendo mwema wa jamii                                |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b> | <b>Umahiri Mkuu</b>                         | <b>Umahiri Mahususi</b>  |
|-----------|-------------|---|--|
| 5.        | Kiswahili   | 5.1 Kumudu stadi za juu za Kiswahili        | 5.1.1 Kukuza uelewa wa misingi na kanuni za Kiswahili<br>5.1.2 Kukuza msamiati kutokana na mazungumzo na maandishi changamani<br>5.1.3 Kutumia msamiati na sarufi stahiki katika miktadha mbalimbali |
|           |             | 5.2 Kuthamini Kiswahili kama lugha ya Taifa | 5.2.1 Kutambua chimbuko na asili ya Kiswahili<br>5.2.2 Kutathmini kukua na kuenea kwa Kiswahili<br>5.2.3 Kutambua matumizi ya lugha ya kwanza, pili, rasmi na lugha ya Taifa                         |
|           |             | 5.3 Kuhariri kazi mbalimbali                | 5.3.1 Kumudu stadi za uhariri  |
|           |             | 5.4 Kutafsiri na kukalimani kazi mbalimbali | 5.4.1 Kutafsiri matini mbalimbali<br>5.4.2 Kukalimani mazungumzo mbalimbali<br>5.4.3 Kutathmini kazi mbalimbali za tafsiri<br>5.4.4 Kutathmini ukalimani   |
|           |             | 5.5 Kuthamini kazi za fasihi                | 5.5.1 Kutambua nadharia ya fasihi<br>5.5.2 Kutathmini maendeleo ya fasihi<br>5.5.3 Kuhakiki kazi za fasihi<br>5.5.4 Kutunga kazi za fasihi   |

| Na | Somo    | Umahiri Mkuu  | Umahiri Mahususi  |
|----|---------|---|---|
| 6. | English | 6.1 Demonstrate mastery of advanced English language skills | 6.1.1 Automate the production of oral descriptions and conversations using standard pronunciation<br>6.1.2 Develop vocabulary from conversation and written texts<br>6.1.3 Use correct grammar and vocabulary in oral and written language tasks  |
|    |         | 6.2 Comprehend oral and written information                 | 6.2.1 Comprehend oral messages with confidence and autonomy<br>6.2.2 Construct complex and stylistic meanings from diverse and multiple texts<br>6.2.3 Demonstrate advanced oral and written proficiency in a variety of communicative contexts<br>6.2.4 Read texts critically to recognise potential implications beyond the author's explicit meaning |
|    |         | 6.3 Communicate effectively in different contexts           | 6.3.1 Manage conversations with a good command of pronunciation<br>6.3.2 Create a variety of complex oral and written texts for different communicative purposes<br>6.3.3 Develop advanced socio-cultural analysis of functional texts  |

| Na | Somo | Umahiri Mkuu  | Umahiri Mahususi  |
|----|------|---|---|
|    |      | 6.4 Provide advanced English language services to the community | 6.4.1 Apply principles of interpretation to provide complex and authentic interpretations<br>6.4.2 Apply principles of translation to produce complex and authentic translation<br>6.4.3 Apply principles of editing and proofreading a variety of texts<br>6.4.4 Manage complex translation and editing projects using Computer-Assisted tools |
|    |      | 6.5 Appreciate and create literary works                        | 6.5.1 Appreciate the aesthetic and value of literature<br>6.5.2 Analyse genres of literature and appreciate their conventions<br>6.5.3 Evaluate the context in which literary texts are written, read and understood<br>6.5.4 Create complex literary works   |

| الكفايات الخاصة<br>Umahiri mahsusi   | الكفايات العامة<br>Umahiri mkuu  | Somo    | Na |
|--|--|---------|----|
| <p>١,١,٧ تطوير فهم مبادئ وقوانين اللغة العربية</p> <p>7.1.1 Kukuza uelewa wa misingi na kanuni za lugha ya Kiarabu.</p> <p>٢,١,٧ تطوير المفردات من المحادثات والنصوص المركبة</p> <p>7.1.2 Kukuza msamiati kutokana na mazungumzo na maandishi changamani</p> <p>٣,١,٧ استخدام المفردات والقواعد المناسبة</p> <p>7.1.3 Kutumia msamiati na sarufi stahiki</p> | <p>١,٧ إتقان مهارات اللغة العربية المتقدمة</p> <p>7.1 Kumudu stadi za juu za lugha ya Kiarabu</p>  | Kiarabu | 7. |
| <p>١,٢,٧ تطوير القدرة على فهم المحادثات في اللغة العربية</p> <p>7.2.1 Kukuza uelewa wa mazungumzo ya Kiarabu</p> <p>٢,٢,٧ تطوير فهم النصوص العربية</p> <p>7.2.2 Kukuza uelewa wa matini andishi za kiarabu</p> <p>٣,٢,٧ تطوير مهارات الاتصال</p> <p>7.2.3 Kukuza stadi za mawasiliano</p>  | <p>٢,٧ إظهار مستوى متقدم من فهم اللغة العربية شفاهة وكتابة.</p> <p>7.2 Kuonesha kiwango cha juu cha uelewa wa Kiarabu katika mazungumzo na maandishi</p> |         |    |
| <p>١,٣,٧ تفسير النصوص المركبة</p> <p>7.3.1 Kutafsiri matini changamani</p> <p>٢,٣,٧ إجراء الترجمة</p> <p>7.3.2 Kufanya ukalimani</p> <p>٣,٣,٧ تحرير النصوص المركبة</p> <p>7.3.3 Kuhariri matini changamani</p>   | <p>٣,٧ التفسير والتحرير و الترجمة</p> <p>7.3 Kutafsiri, kuhariri na kukalimani.</p>  |         |    |

| الكفايات الخاصة<br>Umahiri mahsusi   | الكفايات العامة<br>Umahiri mkuu  | Somo | Na |
|--|--|------|----|
| <p>١, ٤, ٧ تقييم تطور الأدب العربي.</p> <p>7.4.1 Kutathmini maendeleo ya fasihi ya Kiarabu</p> <p>٢, ٤, ٧ نقد أعمال الأدب العربي</p> <p>7.4.2 Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiarabu</p> <p>٣, ٤, ٧ تأليف الأعمال السهلة في الأدب العربي</p> <p>7.4.3 Kutunga kazi sahili za fasihi ya Kiarabu</p> | <p>٤, ٧ تقديم وإبداع أعمال الأدب العربي</p> <p>7.4 Kuthamini na kubuni kazi za fasihi ya Kiarabu</p> |      |    |

| <b>Na</b>  | <b>Somo</b>   | <b>Umahiri Mkuu</b>  | <b>Umahiri Mahususi</b>   |
|--|---|--|---|
| 8.   | Kifaransa   | 8.1 Maîtriser les compétences langagières du français au niveau avancé | 8.1.1 Développer la connaissance grammaticale (morphologie, phonologie, syntaxe, lexicologie, sémantique, et pragmatique)<br>8.1.2 Développer le vocabulaire à travers la conversation et à l'écrit<br>8.1.3 Utiliser le vocabulaire et la grammaire appropriés |
|  |   | 8.2 Démontrer le niveau avancé de comprendre en français               | 8.2.1 Développer la compréhension des conversations en français   |
|  |   |  | 8.2.2 Développer la compréhension des textes complexes en français<br>8.2.3 Maîtriser la communication complexe orale et écrite   |
|  |   | 8.3 Traduire, éditer et interpréter                                    | 8.3.1 Traduire des textes complexes<br>8.3.2 Éditer des textes complexes<br>8.3.3 Interpréter   |
| 8.4 Apprécier et composer des œuvres littéraires | 8.4.1 Lire et comprendre des œuvres littéraires des écrivains francophones<br>8.4.2 Composer des œuvres littéraires en français |  |   |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b> | <b>Umahiri Mkuu</b>   | <b>Umahiri Mahususi</b>   |
|-----------|-------------|---|---|
| 9.        | Kichina     | 9.1 掌握高级汉语技能<br>Kumudu stadi za juu za Kichina  | 9.1.1 提高对汉语基础知识和原则的理解<br>Kukuza uelewa wa misingi na kanuni za lugha ya Kichina<br>9.1.2 拓展汉语词汇<br>Kukuza msamiati wa lugha Kichina<br>9.1.3 在各种语境中, 使用适当的词汇和语法<br>Kutumia msamiati na sarufi stahiki |
|           |             | 9.2 在会话和写作中展现出对汉语的高水平理解<br>Kuonesha kiwango cha juu cha uelewa wa lugha ya Kichina katika mazungumzo na maandishi | 9.2.1 提高对汉语对话和文本的理解<br>Kukuza uelewa wa mazungumzo na matini katika lugha ya Kichina  |
|           |             | 9.3 在对话和写作中进行高水平的交流<br>Kuwasiliana kwa kiwango cha juu kwa mazungumzo na maandishi                                | 9.3.1 展示理解中文对话的能力<br>Kuonesha umahiri wa kuwasiliana kwa mazungumzo<br>9.3.2 展示在各种语境中进行有效写作的能力<br>Kuonesha umahiri wa kuwasiliana kwa maandishi   |
|           |             | 9.4 在各种语境下进行口译和笔译<br>Kutafsiri na kukalimani  | 9.4.1 笔译复杂文本<br>Kutafsiri matini changamani<br>9.4.2 提供口译<br>Kufanya ukalimani  |



| Na  | Somo    | Umahiri Mkuu                                       | Umahiri Mahususi   |
|-----|---------|--|--|
| 10. | Fizikia | 10.1 Kumudu dhana, nadharia na kanuni za kifizikia | 10.1.1 Kukuza uelewa wa dhana, nadharia na kanuni za kifizikia<br>10.1.2 Kutumia vipimo katika fizikia na kubaini kasoro zitokanazo na upimaji ( <i>precision and accuracy</i> )<br>10.1.3 Kuchambua ufaafu wa vifaa na mbinu mbalimbali za upimaji katika fizikia |
|     |         | 10.2 Kufanya majaribio ya kifizikia                | 10.2.1 Kufanya majaribio ya kifizikia  |
|     |         | 10.3 Kufanya kazimradi ya kifizikia                | 10.3.1 Kufanya kazimradi ya kifizikia  |
| 11  | Kemia   | 11.4 Kumudu dhana, nadharia na kanuni za kikemia   | 11.4.1 Kukuza uelewa wa dhana, nadharia na kanuni za kikemia<br>11.4.2 Kukuza uelewa wa mabadiliko ya tabia ya kiumbo na ya kikemia ya vitu kwa kutumia mpangilio wa elementi katika jedwali   |

| Na | Somo             | Umahiri Mkuu   | Umahiri Mahususi   |
|----|------------------|--|--|
|    |                  |  | <p>11.4.3 Kutumia dhana za kemia kupata uelewa wa nguvu za kikemia, mabadiliko na matumizi yake</p> <p>11.4.4 Kukuza uelewa wa dhana na kanuni za <i>Organic Chemistry</i></p> |
|    |                  | 11.5 Kufanya uchunguzi kwa kutumia misingi ya kikemia          | 11.5.1 Kutengeneza kemikali za <i>Carbon</i>   |
|    |                  | 11.6 Kufanya kazimradi ya kikemia                              | 11.6.1 Kufanya kazimradi ya kikemia  |
| 12 | Baiolojia        | 12.7 Kumudu nadharia, kanuni na misingi ya kibaiolojia         | 12.7.1 Kukuza uelewa wa nadharia, kanuni na misingi ya kibaiolojia   |
|    |                  | 12.8 Kuwasiliana kwa kutumia majina na istilahi za kibaiolojia | 12.8.1 Kumudu kanuni za uandishi wa majina ya kibaiolojia na kuainisha makundi ya viumbe hai   |
|    |                  | 12.9 Kufanya uchunguzi wa kibaiolojia                          | <p>12.9.1 Kutumia misingi ya kibaiolojia kuchunguza anatomia na fiziolojia ya viumbe hai</p> <p>12.9.2 Kumudu stadi za kufanya uchunguzi wa kibaiolojia</p>                    |
| 13 | Chakula na Lishe | 13.1 Kumudu misingi ya chakula na lishe                        | 13.1.1 Kuonesha uelewa wa mahitaji ya chakula kwa makundi mbalimbali ya watu   |

| Na | Somo                | Umahiri Mkuu  | Umahiri Mahususi  |
|----|---------------------|---|---|
|    |                     |   | <p>13.1.2 Kufanya uchunguzi wa virutubishi vilivyomo katika aina mbalimbali za vyakula</p> <p>13.1.3 Kuonesha uelewa wa lishe bora na mgawanyo wa chakula katika kaya (<i>intra-household food distribution</i>)</p>  |
|    |                     | 13.2 Kumudu matumizi ya teknolojia kusindika na kuhifadhi vyakula | 13.2.1 Kusindika na kuhifadhi vyakula mbalimbali kwa kutumia vifaa vya kisasa   |
|    |                     | 13.3 Kumudu misingi na kufanya tathmini ya hali ya lishe          | 13.3.1 Kutathmini hali ya chakula na lishe katika jamii   |
|    |                     | 13.4 Kufanya kazimradi katika chakula na lishe                    | 13.4.1 Kufanya kazimradi katika chakula na lishe  |
| 14 | Sayansi ya Kompyuta | 14.1 Kumudu kanuni za msingi za Sayansi ya Kompyuta               | <p>14.4.1 Kuonesha uelewa wa kanuni za usanifu na mpangilio wa utendaji wa kompyuta</p> <p>14.4.2 Kuonesha uelewa wa mitandao ya kompyuta</p> <p>14.4.3 Kumudu utengenezaji wa programu tumizi za wavuti (Kwa kutumia PHP/Python; JavaScript; CSS, n.k)</p> |

| Na | Somo | Umahiri Mkuu                         | Umahiri Mahususi   |
|----|------|--------------------------------------|--|
|    |      |                                      | <p>14.4.4 Kumudu kanuni za msingi za lugha ya programu za komputa inayozingatia vitu ‘Object Oriented’ (Kwa kutumia C++; Java; Python; n.k)</p> <p>14.4.5 Kumudu kanuni za msingi za aligorizimu na miundo ya Data</p> <p>14.4.6 Kuonesha uelewa wa kanuni za mifumo ya uendeshaji ya kompyuta [Aina za Mfumo wa Uendeshaji wa Kompyuta; Usimamizi wa kumbukumbu; Usimamizi wa faili; Upangiliaji wa CPU; n.k]</p>                     |
|    |      | <p>14.2 Kumudu usimamizi wa data</p> | <p>14.2.1 Kumudu kanuni za juu za kanzidata na mifumo ya usimamizi wa kanzidata</p> <p>14.2.2 Kumudu Kanuni za uchambuzi wa data za kompyuta (uchambuzi wa kina, uwasilishaji wa taarifa na tafsiri ya matokeo, n.k)</p> <p>14.2.3 Kuonesha uelewa wa teknolojia kiotomatiki na zinazoibuka [Mifumo otomatiki, Akili Bandia, ‘Mashine learning’, picha za 3D na holographia, Uhalisia Pepe (VR), Uhalisia Ulioboreshwa (AR), n.k.]</p> |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b>     | <b>Umahiri Mkuu</b>                        | <b>Umahiri Mahususi</b>  |
|-----------|-----------------|--|--|
| 15        | Hisabati        | 15.1 Kukuza uelewa wa dhana za kihisabati  | 15.1.1 Kukuza uelewa wa maarifa na stadi za kihisabati<br>15.1.2 Kuonesha uelewa wa msingi wa calculus<br>15.1.3 Kukuza uelewa wa takwimu  |
|           |                 | 15.2 Kumudu nadharia ya seti na mantiki    | 15.2.1 Kukuza uelewa wa nadharia ya seti na mantiki  |
|           |                 | 15.3 Kumudu aljebra                        | 15.3.1 Kukuza uelewa wa aljebra  |
|           |                 | 15.4 Kufanya kazimradi katika hisabati     | 15.4.1 Kufanya kazimradi kwa kutumia hisabati  |
| 16        | Hisabati Tumizi | 16.1 Kutumia hisabati katika fani nyingine | 16.1.1 Kutumia stadi za juu za trigonometry, vectors na geometry kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali<br>16.1.2 Kutumia functions na calculus kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali<br>16.1.3 Kutumia takwimu kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b> | <b>Umahiri Mkuu</b>   | <b>Umahiri Mahususi</b>  |
|-----------|-------------|---|--|
|           |             | 16.2 Kutumia Aljebra na nadharia ya seti na mantiki kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali | 16.2.1 Kutumia nadharia ya seti na mantiki kujenga hoja na kufanya maamuzi<br>16.2.2 Kutumia stadi za mpangilio na mtiririko wa namba katika miktadha mbalimbali<br>16.2.3 Kutumia stadi za aljebra na nadharia namba katika miktadha mbalimbali |
| 17        | Kilimo      | 17.1 Kumudu misingi ya kilimo   | 17.1.1 Kukuza uelewa wa misingi na kanuni za kilimo<br>17.1.2 Kumudu uelewa wa mnyororo wa thamani kwa baadhi ya mazao ya kilimo<br>17.1.3 Kumudu misingi ya matumizi ya teknolojia katika kilimo  |
|           |             | 17.2 Kutumia teknolojia kuongeza tija katika kilimo   | 17.2.1 Kutumia teknolojia kuongeza tija katika kilimo  |
|           |             | 17.3 Kufanya kazimradi ya kilimo  | 17.3.1 Kubuni na kufanya kazimradi ya kilimo   |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b>                     | <b>Umahiri Mkuu</b>   | <b>Umahiri Mahususi</b>  |
|-----------|---------------------------------|---|--|
| 18        | Historia ya Tanzania na Maadili | 18.1 Kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya Taifa             | 18.1.1 Kumudu historia, utambulisho na maadili ya Taifa<br>18.1.2 Kutathmini mchango wa historia na urithi katika kuchangia maendeleo ya Taifa<br>18.1.3 Kutumia fursa mbalimbali zitokanazo na historia na urithi wa Tanzania kujenga ushirikiano na kukuza biashara ya kimataifa           |
|           |                                 | 18.2 Kumudu historia ya Tanzania na maadili kabla ya ukoloni              | 18.2.1 Kutathmini vichocheo vya maendeleo ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni<br>18.2.2 Kuelezea uhusiano wa jamii za Kitanzania na jamii nyingine duniani kabla ya ukoloni<br>18.2.3 Kuhusianisha mapokeo ya mifumo ya kihistoria katika kuelezea maadili ya Kitanzania |
|           |                                 | 18.3 Kumudu historia ya Tanzania na maadili wakati wa ukoloni, 1890 -1960 | 18.3.1 Kutathmini ukoloni kama nguvu laini (soft power) ya kujenga mwelekeo mpya wa jamii<br>18.3.2 Kuchambua mchango wa ukoloni katika mfumo wa maadili ya Kitanzania   |

| Na | Somo | Umahiri Mkuu  | Umahiri Mahususi  |
|----|------|---|---|
|    |      | 18.4 Kumudu historia ya ujenzi wa Taifa na maadili yake katika kipindi cha 1961-1966  | 18.4.1 Kumudu chimbuko la ukoloni mamboleo<br>18.4.2 Kutathmini mabadiliko ya mifumo ya ulinzi na usalama wa Taifa<br>18.4.3 Kuchambua visababishi vya mabadiliko ya sera ya mambo ya nje na uhusiano wa kimataifa<br>18.4.4 Kutathmini mchango wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika kudumisha uhuru, umoja na amani ya kitaifa |
|    |      | 18.5 Kutathmini ujenzi wa Taifa na maadili yake wakati wa Azimio la Arusha, 1967-1985 | 18.5.1 Kuchambua chimbuko la Azimio la Arusha na matokeo yake kiuchumi, kisiasa, kimaadili na kiutamaduni<br>18.5.2 Kutathmini nafasi ya Tanzania katika kujenga uhusiano wa kikanda  |
|    |      | 18.6 Kutathmini historia ya Tanzania na maadili wakati wa uliberali, 1986 hadi sasa   | 18.6.1 Kutafsiri mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimaadili katika kipindi cha uliberali na utandawazi kuanzia 1986 hadi sasa  |
|    |      | 18.7 Kufanya utafiti kuhusu historia ya Tanzania na maadili                           | 18.7.1 Kujenga hoja kuhusu historia ya Tanzania na maadili kwa kutumia ushahidi uliotokana na utafiti   |



| <b>Na</b> | <b>Somo</b>  | <b>Umahiri Mkuu</b>   | <b>Umahiri Mahususi</b>   |
|-----------|--------------|---|---|
| 19        | Michezo      | 19.1 Kumudu historia na umuhimu wa michezo                      | 19.1.1 Kutathmini historia na maendeleo ya michezo Tanzania<br>19.1.2 Kutambua fursa zilizopo katika michezo kitaifa na kimataifa                                   |
|           |              | 19.2 Kuhusianisha fiziolojia na michezo                         | 19.2.1 Kutambua muundo na mifumo ya mwili wa binadamu<br>19.2.2 Kuhusianisha mifumo na mijongeo ya mwili wa binadamu na michezo                                     |
|           |              | 19.3 Kucheza michezo kwa ustadi                                 | 19.3.1 Kumudu mazoezi kwa michezo mahsusi<br>19.3.2 Kujenga stadi za juu katika michezo mahsusi   |
|           |              | 19.4 Kuratibu na kusimamia shughuli mbalimbali za michezo       | 19.4.1 Kujenga misingi ya uongozi, utawala na usimamizi wa michezo  |
|           |              | 19.5 Kufanya kazimradi kuhusu michezo                           | 19.5.1 Kubuni na kufanya kazimradi inayohusu michezo  |
| 20        | Sanaa Sanifu | 20.1 Kukuza uelewa wa dhana, nadharia na kanuni za Sanaa Sanifu | 20.1.1 Kuonesha uelewa wa fomu za sanaa sanifu katika Afrika Mashariki na Afrika Magharibi<br>20.1.2 Kuonesha uelewa wa misingi ya utunzaji wa kazi za sanaa sanifu |

| Na | Somo   | Umahiri Mkuu   | Umahiri Mahususi  |
|----|--------|--|---|
|    |        | 20.2 Kutengeneza kazi za sanaa sanifu                          | 20.2.1 Kutengeneza picha mnato na jongefu<br>20.2.2 Kukuza matumizi ya mbinu mbalimbali kutengeneza kazi za sanaa<br>20.2.3 Kutengeneza maudhui halisi na ya dhahania   |
|    |        | 20.3 Kutumia TEHAMA kubuni na kutengeneza kazi za sanaa sanifu | 20.3.1 Kutumia TEHAMA kubuni na kutengeneza kazi za sanaa sanifu  |
|    |        | 20.4 Kufanya kazimradi ya Sanaa Sanifu                         | 20.4.1 Kuandaa mkoba wa kazi bora za sanaa sanifu   |
| 21 | Muziki | 21.1 Kumudu dhana, nadharia na kanuni za muziki                | 21.1.1 Kukuza uelewa wa dhana, nadharia na kanuni za muziki<br>21.1.2 Kukuza uelewa wa misingi ya muziki  |
|    |        | 21.2 Kufanya kazi za muziki                                    | 21.2.1 Kukuza umahiri wa kutunga muziki kwa lugha mbalimbali<br>21.2.2 Kukuza umahiri wa kuimba nyimbo za kitamaduni na za kigeni<br>21.2.3 Kukuza umahiri wa kupiga ala za muziki za kiasili na za kigeni<br>21.2.4 Kuonesha uelewa wa maadili katika tasnia ya muziki |

| Na | Somo               | Umahiri Mkuu  | Umahiri Mahususi   |
|----|--------------------|---|--|
|    |                    | 21.3 Kutumia TEHAMA katika shughuli za muziki                         | 21.3.1 Kutumia TEHAMA kuzalisha kazi za muziki   |
|    |                    | 21.4 Kufanya kazimradi ya Muziki                                      | 21.4.1 Kubuni na kufanya kazimradi ya muziki   |
| 22 | Sanaa za Maonyesho | 22.1 Kukuza uelewa wa dhana, nadharia na kanuni za Sanaa za Maonyesho | 22.1.1 Kuelezea maendeleo ya sanaa za maonyesho na matapo yake<br>22.1.2 Kuelezea historia na kanuni za uandishi, uigizaji na uongozaji wa kazi za sanaa za maonyesho<br>22.1.3 Kumudu mbinu na kanuni za kubaini maeneo ya kufanyia sanaa za maonyesho<br>22.1.4 Kumudu kanuni za kusimamia matamasha ya sanaa za maonyesho         |
|    |                    | 22.2 Kufanya sanaa za maonyesho                                       | 22.2.1 Kubuni kazi za sanaa za maonyesho kwa ajili ya jukwaa, filamu, redio na televisheni<br>22.2.2 Kuigiza na kuongoza kazi za sanaa za maonyesho za jukwaani, filamu, redio na televisheni<br>22.2.3 Kutumia TEHAMA katika sanaa za maonyesho<br>22.2.4 Kuonesha uelewa wa misingi na kanuni za maadili katika sanaa za maonyesho |

| Na | Somo                     | Umahiri Mkuu   | Umahiri Mahususi  |
|----|--------------------------|--|---|
|    |                          | 22.3 Kumudu matumizi bunifu ya lugha katika sanaa za maonyesho | 22.3.1 Kumudu nadharia na kanuni za matumizi ya lugha ya vitendo katika sanaa za maonyesho<br>22.3.1 Kutumia lugha ya vitendo kuandaa na kuwasilisha kazi za sanaa za maonyesho   |
| 23 | Ushoni                   | 23.1 Kutumia misingi na kanuni za utengenezaji wa mavazi       | 23.1.1 Kumudu sifa na matumizi ya aina mbalimbali za vitambaa ( <i>cloth and garment</i> )<br>23.1.2 Kunakshi vitambaa vya ushoni kwa kutumia mbinu mbalimbali<br>23.1.2 Kubuni mavazi ya asili yanayotumika katika makabila mbalimbali ya Tanzania kwa kuzingatia kanuni za ushonaji |
|    |                          | 23.2 Kutumia TEHAMA katika kubuni na kushona mavazi            | 23.2.1 Kutumia TEHAMA kubuni na kuzalisha mavazi  |
|    |                          | 23.3 Kufanya kazimradi ya Ushoni                               | 23.3.1 Kuandaa mkoba wa kazi wa shughuli mbalimbali za ushoni   |
| 24 | Mawasiliano ya Kitaaluma | 24.1 Kumudu kanuni za lugha ya Kiingereza                      | 24.1.1 Kuonesha uelewa wa kanuni za msingi za lugha ya Kiingereza na matumizi yake<br>24.1.2 Kutumia kanuni za lugha kuunda sentensi, aya na matini   |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b>       | <b>Umahiri Mkuu</b>                                   | <b>Umahiri Mahususi</b>  |
|-----------|-------------------|---|--|
|           |                   | 24.2 Kutumia stadi za mawasiliano ya kitaaluma        | 24.2.1 Kumudu matumizi ya Kiingereza kuwasiliana kitaaluma<br>24.2.2 Kuandaa nyaraka mbalimbali kwa Kiingereza<br>24.2.3 Kutumia TEHAMA kutafuta taarifa za kitaaluma<br>24.2.4 Kuandaa na kufanya mawasilisho ya kitaaluma kwa Kiingereza<br>24.2.5 Kutumia vielelezo kwenye nyaraka za kitaaluma |
| 25        | Elimu ya Biashara | 25.1 Kumudu misingi ya biashara                       | 25.1.1 Kukuza uelewa wa misingi na kanuni za biashara  |
|           |                   | 25.2 Kukuza uelewa wa mazingira ya kuendesha biashara | 25.2.1 Kumudu uelewa wa misingi ya sera na sheria za uendeshaji wa biashara ya kati nchini Tanzania  |
|           |                   | 25.3 Kufanya kazimradi katika biashara                | 25.3.1 Kuandaa mpango wa biashara ya kati (Business plan)  |
| 26        | Uhasibu           | 26.1 Kumudu dhana, nadharia na kanuni za Uhasibu      | 26.1.1 Kuelewa dhana, nadharia na kanuni za Uhasibu<br>26.1.2 Kuandaa mpango kazi wa kahasibu  |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b> | <b>Umahiri Mkuu</b>                                       | <b>Umahiri Mahususi</b>   |
|-----------|-------------|---|---|
|           |             | 26.2 Kuandaa taarifa za kiasibu                           | 26.2.1 Kumudu utunzaji wa mahesabu ya biashara<br>26.2.2 Kubaini makosa katika miamala ya kibiashara na kuyarekebisha<br>26.2.3 Kutumia kanuni za uhasibu |
|           |             | 26.3 Kumudu miongozo na maadili ya taaluma ya uhasibu     | 26.3.1 Kumudu kanuni na miongozo ya maadili ya uhasibu  |
|           |             | 26.4 Kumudu matumizi ya TEHAMA kuchambua taarifa za fedha | 26.4.1 Kutumia programu za kompyuta kufanya uchambuzi wa kifedha  |
| 27        | Uchumi      | 27.1 Kumudu dhana, nadharia na kanuni za Uchumi           | 27.1.1 Kumudu dhana, nadharia na kanuni zinazotumika katika Uchumi<br>27.1.2 Kumudu uchambuzi wa hali ya uchumi   |
|           |             | 27.2 Kufanya kazimradi ya kiuchumi                        | 27.2.1 Kubuni na kufanya kazimradi ya kiuchumi  |

| <b>Na</b> | <b>Somo</b>         | <b>Umahiri Mkuu</b>                    | <b>Umahiri Mahususi</b>   |
|-----------|---------------------|--|---|
| 28        | Fasihi ya Kiswahili | 28.1 Kumudu dhana na misingi ya fasihi | 28.1.1 Kukuza uelewa wa dhana ya fasihi<br>28.1.2 Kutathmini nadharia za chimbuko la fasihi<br>28.1.3 Kuchambua uhusiano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi<br>28.1.4 Kuhusianisha fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa Kiswahili<br>28.1.5 Kutathmini maendeleo ya fasihi kitaifa na kimataifa |
|           |                     | 28.2 Kuthamini kazi za fasihi          | 28.2.1 Kuonesha uelewa wa misingi ya kutathmini kazi za fasihi<br>28.2.2 Kutathmini nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi<br>28.2.3 Kuhakiki kazi za fasihi kwa kutumia misingi na nadharia mbalimbali<br>28.2.4 Kutumia fasihi kutathmini maadili na mitazamo katika jamii                         |
|           |                     | 28.3 Kujenga ujumi                     | 28.3.1 Kumudu mbinu zinazotumika kujenga ujumi katika kazi za fasihi<br>28.3.2 Kutathmini maana mbalimbali za kazi za fasihi<br>28.3.3 Kutumia fasihi kujenga hoja zenye mantiki na ushawishi   |

| Na | Somo                  | Umahiri Mkuu  | Umahiri Mahususi  |
|----|-----------------------|---|---|
|    |                       | 28.4 Kubuni kazi changamani za fasihi                                 | 28.4.1 Kutambua fursa zinazotokana na kazi za fasihi ya Kiswahili<br>28.4.2 Kumudu kanuni za utunzi wa kazi za fasihi<br>28.4.3 Kutunga kazi za fasihi  |
| 29 | Literature in English | 29.1 Demonstrate mastery of the concepts and principles of literature | 29.1.1 Demonstrate a broad understanding of the concepts of literature<br>29.1.2 Evaluate theories of the origin and development of literature nationally and internationally<br>29.1.3 Explain the origin and development of African literature in English<br>29.1.4 Assess the contribution of Tanzanian writers to the development of Tanzanian literature in English<br>29.1.5 Analyse the relationship between folklore and written literature |
|    |                       | 29.2 Appreciate literary works  | 29.2.1 Exhibit an in-depth understanding of elements of literature<br>29.2.2 Analyse literary criticism theories<br>29.2.3 Analyse critically pre-colonial, colonial, liberation and post-colonial literatures<br>29.2.4 Analyse the nexus between literature and politics, aesthetics and social inequalities  |



| Na | Somo | Umahiri Mkuu                                     | Umahiri Mahususi   |
|----|------|--|--|
|    |      | 29.3 Demonstrate mastery of argumentative skills | 29.3.1 Evaluate the effectiveness of various elements of form in shaping meaning<br>29.3.2 Use literary works to build rational arguments and judgements<br>29.3.3 Use literature to adapt and manage new communicative contexts |
|    |      | 29.4 Create literary works                       | 29.4.3 Demonstrate mastery of the principles of composing literary works<br>29.4.3 Identify opportunities created by literary works<br>29.4.3 Compose original literary works  |

### 3.3 Maeneo ya Ujifunzaji na Tahasusi za Kidato cha V-VI

Tahasusi katika Kidato cha V na VI zimegawanywa katika maeneo saba ya ujifunzaji ya Sayansi ya Jamii, Lugha, Elimu ya Biashara, Sayansi, Michezo, Sanaa na Elimu ya Dini. Idadi na aina ya tahasusi zitapitiwa mara kwa mara kuhakikisha zinakidhi mahitaji halisi ya Taifa katika wakati husika. Ili kuongeza wigo wa fursa za kujiunga na elimu ya juu, idadi ya masomo katika kila tahasusi haitakuwa chini ya matatu na haitazidi manne kulingana na uwezo na malengo ya mwanafunzi. Aidha, aina ya masomo katika kila tahasusi, imezingatia malengo ya kitaalamu (*career aspirations and pathways*) ya wahitimu na rasilimali zitakazokuwepo shuleni. Pia, mwanafunzi wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V na VI ataruhusiwa kuchagua masomo ya ziada, yakiwemo yale ya Mkondo wa Elimu ya Amali, kulingana na ratiba na uwezo wa shule husika ili kujiongezea umahiri utakaomwezesha kumudu maisha yake baada ya kuhitimu. Maeneo ya ujifunzaji na tahasusi zimebainishwa katika Jedwali Namba 3.

**Jedwali 3: Maeneo ya Ujifunzaji na Tahasusi za Kidato cha V-VI**

| <b>Eneo la Ujifunzaji</b> | <b>Na</b>                              | <b>Masomo</b>                                      | <b>Tahasusi</b>       |
|---------------------------|--|--|-----------------------|
| Sayansi ya Jamii          | 1.                                     | History, Geography and Kiswahili                   | HGK                   |
|                           | 2.                                     | History, Geography and English Language            | HGL                   |
|                           | 3.                                     | History, Geography and French                      | HGF                   |
|                           | 4.                                     | History, Geography and Arabic                      | HGAr                  |
|                           | 5.                                     | History, Geography and Chinese                     | HGCh                  |
|                           | 6.                                     | History, Geography and Fasihi ya Kiswahili         | HGFa                  |
|                           | 7.                                     | History, Kiswahili and English Language            | HKL                   |
|                           | 8.                                     | History, Geography and Literature in English       | HGLi                  |
|                           | 9.                                     | History, Geography and Economics                   | HGE                   |
| Lugha                     | 10.                                    | Kiswahili, English Language and French             | KLF <sup>1</sup>      |
|                           | 11.                                    | Kiswahili, English Language and Arabic             | KLAr <sup>1</sup>     |
|                           | 12.                                    | Kiswahili, English Language and Chinese            | KLCh <sup>1</sup>     |
|                           | 13.                                    | Kiswahili, Arabic and Chinese                      | KArCh <sup>1</sup>    |
|                           | 14.                                    | Kiswahili, Arabic and French                       | KArF <sup>1</sup>     |
|                           | 15.                                    | English Language, French and Arabic                | LFAr <sup>1</sup>     |
|                           | 16.                                    | English Language, French and Chinese               | LFCh <sup>1</sup>     |
|                           | 17.                                    | French, Arabic and Chinese                         | FArCh <sup>1</sup>    |
|                           | 18.                                    | History, English Language and French               | HLF <sup>1</sup>      |
|                           | 19.                                    | History, English Language and Arabic               | HLAr <sup>1</sup>     |
|                           | 20.                                    | History, English Language and Chinese              | HLCh <sup>1</sup>     |
| 21.                       | French, English Language and Economics | FLE  |                       |
| Elimu ya Biashara         | 22.                                    | Economics, Business Studies and Accountancy        | EBuAc** <sup>1</sup>  |
|                           | 23.                                    | Economics, Geography and Mathematics               | EGM                   |
|                           | 24.                                    | Economics, Computer Science and Mathematics        | ECsM <sup>1</sup>     |
|                           | 25.                                    | Business Studies, Accountancy and Computer Science | BuAcCs** <sup>1</sup> |

| <b>Eneo la Ujifunzaji</b> | <b>Na</b> | <b>Masomo</b>   | <b>Tahasusi</b>    |
|---------------------------|-----------|---|--------------------|
|                           | 26.       | Business Studies, Accountancy and Mathematics             | BuAcM <sup>1</sup> |
|                           | 27.       | Business Studies, English Language and French             | BuLF               |
|                           | 28.       | Economics, Business Studies and Elimu ya Dini ya Kiislamu | EBuI               |
|                           | 29.       | Economics, Business Studies and Divinity                  | EBuD               |
| Sayansi                   | 30.       | Physics, Chemistry and Mathematics                        | PCM                |
|                           | 31.       | Physics, Chemistry and Biology                            | PCB**              |
|                           | 32.       | Physics, Geography and Mathematics                        | PGM                |
|                           | 33.       | Physics, Mathematics and Computer Science                 | PMCs <sup>1</sup>  |
|                           | 34.       | Chemistry, Biology and Agriculture                        | CBA** <sup>1</sup> |
|                           | 35.       | Chemistry, Biology and Food and Human Nutrition           | CBN** <sup>1</sup> |
|                           | 36.       | Chemistry, Biology and Geography                          | CBG                |
| Michezo                   | 37.       | Biology, Food and Human Nutrition and Sports              | BNS <sup>1</sup>   |
|                           | 38.       | Kiswahili, Literature in English and Music                | KLiMu <sup>1</sup> |
|                           | 39.       | Kiswahili, English Language and Sports                    | KLS                |
|                           | 40.       | Sport, Arabic and English Language                        | SArL               |
|                           | 41.       | Fasihi ya Kiswahili, English Language and Sports          | FaLS               |
| Sanaa                     | 42.       | Kiswahili, English Language and Theatre Arts              | KLT <sup>1</sup>   |
|                           | 43.       | Kiswahili, French and Theatre Arts                        | KFT <sup>1</sup>   |
|                           | 44.       | Fasihi ya Kiswahili, English Language and Theatre Arts    | FaLT <sup>1</sup>  |
|                           | 45.       | Kiswahili, Literature in English and Theatre Arts         | KLiT <sup>1</sup>  |
|                           | 46.       | Kiswahili, English Language and Music                     | KLMu <sup>1</sup>  |
|                           | 47.       | Kiswahili, French and Music                               | KFMu <sup>1</sup>  |
|                           | 48.       | Fasihi ya Kiswahili, English Language and Music           | FaLMu <sup>1</sup> |
|                           | 49.       | Kiswahili, English Language and Fine Art                  | KLFi <sup>1</sup>  |
|                           | 50.       | Kiswahili, French and Fine Art                            | KFFi <sup>1</sup>  |

| <b>Eneo la Ujifunzaji</b> | <b>Na</b> | <b>Masomo</b>   | <b>Tahasusi</b>      |
|---------------------------|-----------|---|----------------------|
|                           | 51.       | Fasihi ya Kiswahili, English Language and Fine Art              | FaLFi <sup>1</sup>   |
|                           | 52.       | English Language, Chinese and Music                             | LChMu                |
|                           | 53.       | Kiswahili, Literature in English and Fine Art                   | KLiFi <sup>1</sup>   |
|                           | 54.       | Kiswahili, Textile and Garment Construction and Fine Art        | KTeFi <sup>1</sup>   |
|                           | 55.       | English Language, Textile and Garment Construction and Fine Art | LTeFi <sup>1</sup>   |
|                           | 56.       | Arabic, Textile and Garment Construction and Fine Art           | ArTeFi <sup>1</sup>  |
|                           | 57.       | Chinese, Textile and Garment Construction and Fine Art          | ChiTeFi <sup>1</sup> |
| Elimu ya Dini             | 58.       | Elimu ya Dini ya Kiislamu, History and Geography                | IHG                  |
|                           | 59.       | Divinity, History and Geography                                 | DHG                  |
|                           | 60.       | Elimu ya Dini ya Kiislamu, History and Arabic                   | IHAr                 |
|                           | 61.       | Divinity, History and English Language                          | DHL                  |
|                           | 62.       | Elimu ya Dini ya Kiislamu, History and English Language         | IHL                  |
|                           | 63.       | Divinity, History and Kiswahili                                 | DHK                  |
|                           | 64.       | Elimu ya Dini ya Kiislamu, History and Kiswahili                | IHK                  |
|                           | 65.       | Divinity, Kiswahili and English Language                        | DKL                  |
| Amali                     | 66.       | Mathematics, Economics and Business Studies                     | MEBu                 |
|                           | 67.       | Economics, Computer Science and Mathematics                     | ECsM                 |
|                           | 68.       | Business Studies, Economics and English Language                | BuEL                 |
|                           | 69.       | Tourism, English Language and French                            | TLF                  |
|                           | 70.       | Geography, Tourism and Kiswahili                                | GTK                  |
|                           | 71.       | Geography, Tourism and English Language                         | GTL                  |
|                           | 72.       | Geography, Tourism and Arabic                                   | GTAr                 |
|                           | 73.       | Geography, Tourism and Chinese                                  | GTCh                 |

| <b>Eneo la Ujifunzaji</b> | <b>Na</b> | <b>Masomo</b>                              | <b>Tahasusi</b> |
|---------------------------|-----------|--|-----------------|
|                           | 74        | History, Tourism and English Language      | HTL             |
|                           | 75        | History, Tourism and French                | HTF             |
|                           | 76        | History, Tourism and Arabic                | HTAr            |
|                           | 77        | History, Tourism and Chinese               | HTCh            |
|                           | 78        | Agriculture, Biology and Economics         | ABE             |
|                           | 79        | English Language, Music and Chinese        | LMuCh           |
|                           | 80        | English Language, Music and Arabic         | LMuAr           |
|                           | 81        | Business Studies, Economics and French     | BuEF            |
|                           | 82        | Business Studies, Economics and Chinese    | BuECh           |
|                           | 83        | Business Studies, Economics and Arabic     | BuEAr           |
|                           | 84        | English Language, Theatre Arts and French  | LTF             |
|                           | 85        | English Language, Theatre Arts and Chinese | LTCh            |
|                           | 86        | English Language, Theatre Arts and Arabic  | LAr             |
|                           | 87        | French, English Language and Sports        | FLS             |
|                           | 88        | English Language, Chinese and Sports       | LChS            |

\* *Mwanafunzi pia anaweza kuchukua somo lolote moja la ziada kutoka nje ya tahasusi yake. Aidha, kila mwanafunzi atatakiwa kusoma masomo ya Historia ya Tanzania na Maadili na Academic Communication.*

\*\* *Mwanafunzi lazima achukue pia Basic Applied Mathematics au awe amefaulu Additional Mathematics katika Mthani wa Kuhitimu Kidato cha Nne.*

<sup>1</sup>*Tahasusi zinazomtayarisha mwanafunzi kuweza kujiajiri/kuajiriwa mara tu baada ya kuhitimu.*

# Sehemu ya Nne

## Ufundishaji na Ujifunzaji

Utekelezaji wa mtaala huu utahusisha matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kumfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezesaji. Mwalimu atatumia mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wake. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na matumizi ya michezo na sanaa, TEHAMA na teknolojia zingine saidizi, majaribio ya kisayansi, ziara za kimasomo, majadiliano, matembezi darasani na mbinu zingine shirikishi zinazohamasisha ujifunzaji. Mtaala unasisitiza mwalimu kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia zana halisi zinazopatikana katika mazingira yake na kutengeneza mazingira ya mwanafunzi kutumia zana hizo katika miktadha ya ujifunzaji.

Masuala mtambuka ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyozingatiwa katika mtaala huu. Wanafunzi watajifunza masuala mtambuka kama vile mazingira, afya, elimu jumuisi, elimu ya jinsia, elimu ya amani, maadili, haki na wajibu wa mtoto, haki za binadamu, ulinzi na usalama, usalama barabarani, elimu ya fedha, elimu ya rushwa, ushirika na masuala ya muungano. Masuala haya yatachopekwa kwenye masomo bebezi wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji wa masomo mbalimbali kwa kuzingatia uhusiano wa suala mtambuka na somo husika.

### 4.1 Muda na idadi ya vipindi

Mwaka wa masomo utakuwa siku 194 sawa na wiki 39 ambazo zimegawanyika katika mihula miwili inayolingana. Katika kila mihula wiki mbili zitatumika kwa upimaji wa mwisho wa mihula. Mgawanyiko wa vipindi na muda kwa kila somo umefafanuliwa katika Jedwali 4.

**Jedwali 4:** Mgawanyo wa Muda na Vipindi

| Na. | Masomo           | Muda       | Idadi ya Vipindi |
|-----|------------------|------------|------------------|
|     | Somo la Tahasusi | Dakika 400 | 10               |
|     | Somo la Ziada    | Dakika 160 | 4                |
|     | Dini             | Dakika 80  | 2                |

### 4.2 Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia

*Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014* Toleo la Mwaka 2023 inaelekeza matumizi ya lugha ya Kiswahili, Kingereza, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) pamoja na lugha nyingine za kigeni katika elimu na mafunzo. Aidha, Sera inatamka kuwa lugha ya Kingereza itatumika kufundishia na kujifunzia katika elimu ya sekondari. Aidha, masomo ya Kiswahili, *English language*, *French language*, *Chinese language* na *Arabic language* yatafundishwa kwa lugha husika.

## Sehemu ya Tano

### Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Upimaji katika elimu hufanyika kwa lengo la kujua maendeleo ya mwanafunzi kwa kutambua kile anachokijua, anachoweza kufanya, mabadiliko ya tabia na mwelekeo na kubaini changamoto anazokumbana nazo katika kujifunza ili kuzitafutia ufumbuzi. Aidha, upimaji ukitumika vyema huamsha ari ya mwanafunzi kujifunza zaidi na kuboresha ufundishaji. Kama ilivyobainishwa katika *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, mtaala huu unalenga kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Mtaala huu unasisitiza mfumo wa upimaji unaozingatia vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa maendeleo ya kila siku ya mwanafunzi. Tathmini itafanyika ili kubaini kama ujenzi wa umahiri pamoja na stadi za Karne ya 21 ikiwemo kuwajengea wanafunzi ubunifu, fikra tunduizi na uwezo wa kutatua matatizo umefanikiwa. Upimaji wa ndani utaratibiwa shuleni sambamba na ufundishaji na ujifunzaji, na upimaji wa nje utaratibiwa na kutekelezwa na mamlaka husika zikiwemo Baraza la Mitihani la Tanzania na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi ili kuhakikisha uthabiti na kuaminika kwa upimaji wa ndani.

#### 5.1 Upimaji endelevu

Upimaji endelevu hufanyika wakati wote wa ujifunzaji na ufundishaji ndani na nje ya darasa. Upimaji huu humsaidia mwalimu kubaini ufanisi katika utendaji wa shughuli mbalimbali za kila siku za mwanafunzi. Pia, upimaji huu humwezesha mwalimu na mwanafunzi kujua ni eneo gani amefanikiwa au hajafanikiwa ili kuweka mkakati wa kuboresha na kuimarisha ujifunzaji. Vilevile, upimaji huu utamwezesha mwalimu kubaini vipaji mbalimbali vya mwanafunzi kama vile ubunifu, uchoraji, sanaa na michezo. Upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wa mwisho wa Kidato cha VI. Mchanganuo wa alama za upimaji endelevu umeainishwa katika Jedwali 4.

#### Jedwali 5: Mchanganuo wa alama za upimaji endelevu

| Aina ya Upimaji         | Kidato cha V | Kidato cha VI |
|-------------------------|--------------|---------------|
| Mtihani wa muhula wa I  | 5%           | 6%            |
| Mtihani wa muhula wa II | 5%           | -             |
| Kazimradi               | -            | 7%            |
| Mtihani wa Utamilifu    | -            | 7%            |
| <b>Jumla</b>            | <b>30%</b>   |               |

#### 5.2 Upimaji tamati

Upimaji tamati utafanyika mwishoni mwa kila mwezi, muhula na Kidato cha VI. Upimaji wa mwisho wa Kidato cha VI unalenga kupata taarifa na uelewa wa kiwango cha umahiri ambacho mwanafunzi amefikia. Pia, upimaji huu utasaidia kubaini ni kwa

kiasi gani malengo katika ngazi ya Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI yamefikiwa. Ili mwanafunzi ahitimu Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI anatakiwa afanye mtihani wa taifa mwishoni mwa Kidato cha VI. Baraza la Mitihani la Tanzania litahusika na upimaji huu na muhitimu atapata cheti kuonesha kuwa amehitimu hatua hii. Upimaji huu utachangia asilimia 70 ya upimaji wote.

### **5.3 Zana na mbinu za upimaji na tathmini**

Zana na mbinu mbalimbali za upimaji zitatumika kupima nadharia na vitendo katika tendo zima la ujifunzaji na ufundishaji. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na binguabongo, uchunguzi, majaribio, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi) na kazimradi. Mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mitihani ya mwisho. Aidha, mtaala unasisitiza kutumia zana za upimaji kama vile orodhahakiki, dodoso na mkoba wa kazi. Matumizi ya mbinu na zana hizi yatatofautiana kulingana na sababu za upimaji, aina na mahitaji ya somo, mahitaji anuai ya mwanafunzi na umahiri unaokusudiwa kujengwa.



## **Sehemu ya Sita**

### **Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala**

Rasilimali za utekelezaji wa mtaala zinahusisha rasilimali watu, vitu, muda na fedha. Viwango na sifa stahiki za rasilimali hizi zinatolewa na wizara yenye dhamana kupitia miongozo mbalimbali. Baadhi ya rasilimali hizo zimefafanuliwa katika vipengele vya rasilimali watu na vitu, samani na majengo, rasilimali muda na fedha.

#### **6.1 Rasilimali watu**

Rasilimali watu inayohitajika katika utekelezaji wa mtaala inajumuisha walimu mahiri na watumishi wasio walimu (wafanyakazi mweka). Aidha, mwalimu atakayefundisha Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI anatakiwa awe angalau na Shahada ya Ualimu kutoka chuo kinachotambulika na Serikali kwa masomo atakayofundisha. Mwalimu anatakiwa aweze kufundisha, kupima na kufanya tathmini. Sifa zaidi za mwalimu zimefafanuliwa kwenye Kiunzi cha Umahiri wa Mwalimu kilichoandaliwa na wizara inayohusika na elimu.

Watumishi mweka ni watumishi waendeshaji wasiokuwa walimu. Watumishi hawa ni kiungo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa mtaala huu. Kundi hili linajumuisha wataalamu kama vile wakutubi, wataalamu wa maabara, matabibu na wauguzi, makatibu muhtasi na wengine. Wafanyakazi hawa watapaswa kuwa wamepata mafunzo katika chuo kinachotambulika na serikali na wamefuzu katika fani inayohusika.

#### **6.2 Rasilimali vitu**

Rasilimali vitu inahusisha vifaa mbalimbali vitakavyosaidia utekelezaji wa mtaala. Rasilimali hizo ni pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambavyo vinajumuisha mihtasari, miongozo, vitabu vya kiada na ziada na zana za kufundishia na kujifunzia. Vifaa vingine ni vifaa vya sayansi na TEHAMA kama vile vifani, vinasu sauti na kompyuta. Aidha, rasilimali vitu inajumuisha viwanja vya michezo, vifaa vya michezo, sanaa na fani mbalimbali. Vilevile, vifaa vingine muhimu kwa utekelezaji wa mtaala ni vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Vifaa hivyo ni vile vya kusaidia kuona, kusikia na kugusa kama vile mashine za Breli, vitabu vya sauti, vikuza sauti na vikuza maandishi kwa wenye uoni hafifu. Ili kuthibiti ubora, vifaa vitakavyotumika shuleni ni vile vilivyothibitishwa na Wizara inayohusika na elimu.

#### **6.3 Samani na majengo**

Samani na majengo ni miongoni mwa rasilimali muhimu katika utekelezaji wa mtaala. Majengo yanajumuisha madarasa, maabara, karakana, maktaba, ofisi za walimu, mabweni, kumbi, jengo la kutolea huduma za afya na jiko. Samani na majengo hayo yazingatia wanafunzi wa aina zote wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hivyo, samani na majengo yatazingatia mwongozo uliowekwa na Wizara inayohusika na elimu.

#### **6.4 Rasilimali muda**

Muda wa utekelezaji wa mtaala huu ni miaka miwili (2) yenye mihula miwili (2) kwa kila mwaka wa masomo. Siku za masomo kwa mwaka ni 194 ambazo ni sawa na wiki 39 kama ilivyofafanuliwa Sehemu ya Nne katika Jedwali 4. Aidha, kalenda ya masomo itatolewa na wizara yenye dhamana ya kusimamia elimu. Hivyo, wazazi, walezi, jamii, serikali na wadau mbalimbali wa elimu wanatakiwa kuhakikisha kuwa muda uliopangwa unatumika vema katika kutekeleza mtaala huu.

#### **6.5 Rasilimali fedha**

Utekelezaji wa mtaala utategemea uwepo wa rasilimali fedha za kutosha. Rasilimali hii itapatikana kupitia uchangiaji wa fedha na mali kutoka kwa wadau mbalimbali. Serikali itashirikiana na sekta binafsi pamoja na wabia wa maendeleo ya elimu katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na rasilimali fedha yakutosha ili kufanikisha utekelezaji wa mtaala huu

#### **6.6 Ushiriki wa Wadau katika Utekelezaji wa Mtaala**

Ushirikishwaji wa wazazi/walezi na wadau wengine wa elimu ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa mtaala huu . Shule za sekondari zitashirikiana na wadau hawa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa elimu ya sekondari.

#### **6.7 Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mtaala**

Usimamizi wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI ni mchakato muhimu wa kuhakikisha kuwa malengo yake yametekelezwa kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa. Bodi ya Shule, Maafisa Elimu Mkoa, Wilaya na Wathibiti Ubora wa Shule wa Kanda na Wilaya. Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari, Kidato cha V-VI unalenga kuona au kupata mrejesho wa namna mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unavyofanyika ikihusisha mafanikio, changamoto na namna yakuzitatua ili kupata matarajio yaliyokusudiwa.

## Bibliografia

- Africa Union Commission. (2017). *Agenda 2063-The Africa We Want*. (Popular version).
- Charter, A. (1990). *African Charter on the Rights and Welfare of the Child*. AU.
- United Nations. (2016). *Transforming our world: the 2030 agenda for sustainable development*. U.N.
- Halinen, I., & Järvinen, R. (2008). *Towards inclusive education: the case of Finland*. *Prospects*, 38(1), 77-97.
- Hunt, P. F. (2011). Salamanca Statement and IDEA 2004: possibilities of practice for inclusive education. *International Journal of Inclusive Education*, 15(4), 461-476.
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (1982). *Mfumo wa elimu Tanzania 1981-2000. ripoti na maendeleo ya Tume ya Rais ya Elimu*. Juzuu la Pili.
- Kenya Institute of Curriculum Development. (2017). *Special needs education competency-based curriculum materials*.
- Kopweh, P. S. (2014). Curriculum development in Tanzania: an investigation of the formulation, management and implementation of the 2005 curriculum reform in selected disadvantaged districts (*Doctoral dissertation*, University of Glasgow). [https://theses.gla.ac.uk/5774/1/2014\\_kopwehphd.pdf](https://theses.gla.ac.uk/5774/1/2014_kopwehphd.pdf)
- Lakkala, S., Uusiautti, S., & Määttä, K. (2016). How to make the neighbourhood school a school for all? Finnish teachers' perceptions of educational reform aiming towards inclusion. *Journal of Research in Special Educational Needs*, 16 (1), 46-56.
- Mauritius Institute of Education. (2015). *National curriculum framework nine year continuous*. MIE.
- Ministry of Education and Vocational Training. (2014). *Education and training policy*, MoEC.
- Ministry of Education, Science and Technology. (2022). *National strategy for inclusive education in Tanzania 2021/22 -2025/26*. MoEST.
- Ministry of Education, Science and Technology. (2022). *National curriculum framework for basic and teacher education*. Tanzania Institute of Education.
- MoEVT. (2009). *National strategy on inclusive education 2009 – 2017*. MoEST.
- Mushi, P. A. K. (2009). *History and development of education in Tanzania*. African books collective.
- National Institute for Educational Development. (2016). *National curriculum for basic*

- education*. Ministry of Education, Arts and Culture. Windhoek-Republic of Namibia.
- Nyerere J. K. (1967). *Education for self-reliance*. Government printer.
- OECD. (2011). *Building a High Quality Teaching profession: Lessons from around the World*. Paris: OECD publishing.
- Persekutuan, P. P. K. (2013). *Malaysia education blueprint 2013-2025* (Preschool to Post-Secondary Education). Kementerian Pendidikan Malaysia.
- Tanzania Institute of Education. (2007). *Curriculum for advanced level secondary education in Tanzania*. TIE.
- Taasisi ya Elimu Tanzania. (2022). *Ripoti ya maoni ya wadau kuhusu uboreshaji wa mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu*. Taasisi ya Elimu Tanzania.
- The United Republic of Tanzania. (1999). *The Tanzania Development Vision 2025*.
- The United Republic of Tanzania. (2019). *National curriculum framework for basic and teacher education*. Ministry of Education, Science and Technology.
- UNESCO World Education Forum Declaration.(2015). *Education 2030: towards inclusive and equitable quality education and lifelong learning for all: 19–22 May 2015*.